

**TAARIFA YA MAADHIMISHO YA TAMASHA LA PILI LA UTALII  
WILAYA YA NYASA 2017 KWA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA  
MUUNGANO WA TANZANIA MHE. KASSIM MAJALIWA  
MAJALIWA (MB) TAREHE 06 JANUARI 2018.**

**Mhe. Waziri Mkuu,,**

Awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana tena mwaka huu 2018 na kuadhimisha tamasha hili la pili la utalii, aidha tunakushukuru sana wewe binafsi kwa kutenga muda wako na kuamua kushiriki nasi hapa leo tunasema asante na karibu sana Nyasa.

**Mhe. Waziri Mkuu,,**

Tamasha la Utalii Wilaya ya Nyasa liliiasiwa rasmi mwaka 2016 lengo kuu ni kuitangaza Wilaya Nyasa kuibua fursa za utalii na uwekezaji katika nyanja anuai kama kilimo, biashara, uvuvi, uchukuzi na uwekezaji wa viwanda na uboreshajii wa miundombinu.

Hili ni tamasha la pili kufanyika tokea kuasiwi kwake likiwa limebeba kauli mbiu nayosema **“Tangaza Utalii na fursa za uwekezaji Nyasa kuelekea uchumi wa viwanda”** lengo lake kuu ni kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika viwanda kama ambavyo serikali yetu ya awamu ya tano chini ya Rais wetu mpandwa **Mh.Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** imekuwa ikisisitiza.

**Mhe. Waziri Mkuu,,**

Kwa mwaka huu wa pili wa Tamasha la utalii, Wilaya ya Nyasa imefanya utambuzi wa kina wa vivutio vya utalii na fursa mbalimbali za uwekezaji ambazo imeweka mkakati madhubuti wa kuzitangaza kwa wadau wa ndani na nje na kutekeleza agizo lako ulilolitoa wakati wa kuahirisha Bunge la 11 na kuitangaza kanda ya kusini kuwa kitovu cha utalii.

Agizo lako hilo, kwetu tunalionia ni fursa nzuri na adimu, hivyo Wilaya ya Nyasa kama sehemu ya eneo la kusini tunao wajibu wa kuhakikisha tunaitangaza kwa hali na mali.

**Mhe. Waziri Mkuu,,**

Ziwa Nyasa linapatikana Kusini – Magharibi mwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ziwa Nyasa ni la 9 kwa ukubwa duniani ni la tatu kwa ukubwa Afrika, lina kina cha kati ya mita 426 na 758 na hii ni kutokana na kupitiwa na bonde la ufa. Kwa upande wa Tanzania mito mingi inapatikana ikitokea katika safu za milima ya Livingstone, mito hiyo ni

Ruhuhu, Lumeme, Ruhekei, Lwika, Mbamba Bay, Likumbo, Chiwindi n.k ambayo huingiza maji ndani ya Ziwa Nyasa.

Ziwa Nyasa ni kuvutio kikubwa cha Utalii kwa ukanda huu kwa kuwa limesheheni vitu vingi ndani yake na tabia tofauti ukilinganisha na maziwa mengine ya hapa nchini na kwingineko. Baadhi ya tabia za ziwa hili ni uwepo wa maji meupe na maangavu eneo lote la ziwa, mawe marefu ambayo yanajulikana kwa majina ya **hia na mala** yanayobeba sifa tofauti.

Tabia nyingine ni kuwa na mawimbi makubwa, fukwe nzuri na zeny sifa tofauti, mawe kuonekana kama sakafu eneo la Chiwindi, fukwe zeny udongo wa mfinyanzi, kina cha maji kuwa kifupi kwa umbali mrefu, mchanga mdogo ambao watu wa kale walitumia kusugulia meno ili yawe meupe, pia kwa kufua chuma haya yote yanapatikana kwenye fukwe ya Mtipwili na maeneo mengine huota nyasi ambazo zinaonekana kama zimefyekwa kwa ustadi, na fukwe za eneo la Mhalo zina mapango ambayo kuta zake ni kama zimesakafiwa.

Asilimia 15% ya aina za samaki wa maji baridi duniani wanapatikana ziwa Nyasa ambapo kuna aina ya samaki tofauti zaidi ya 600 kutokana na ripoti ya utafiti wa 2011. Ziwa Nyasa lina aina ya samaki wa mapambo zaidi ya 400 na viumbe wengineo ambao hawapatikani katika ziwa lolote duniani hawa wanapatikana katika maeneo tofauti kutegemeana na aina na usalama wa maisha yao. Tangu mwaka 1960 samaki hai wa mapambo walanza kuuzwa katika nchi za Ulaya na Marekani, ambapo nchi nyingi kama vile Japani, Swedeni, Uturuki, Denmark, Canada, Ufaransa, Uingereza na Ujerumanil zilivutiwa na samaki wa mapambo kutoka ziwa Nyasa kutokana na kuwa na sifa ya kipekee yaani rangi nzuri za kupendeza na hakuna sehemu nyingine wanapatikana samaki wa mapambo wa aina hii.

Ziwa hili pia limesheheni utajiri mkubwa wa viumbe hai wakiwemo fisimaji, mamba, nyoka, viboko ambao ni kivutio kikubwa cha utalii.

Ndege wanao hamia kutoka Ulaya na baadhi ya nchi za Afrika wanapatikana maeneo ya mwambao mwa ziwa Nyasa ambo ni kivutio kikubwa cha utalii. Ndenge hao huja kwa ajili ya kujipatia chakula cha aina mbalimbali katika mwambao wa ziwa wakiwa kwenye misafara yao.

Mandhari inayozunguka ziwa hili ambayo inabeba jina la "Mbamba bay," Mbamba ikiwa na maana ya radi na bay ikimaanisha Ghuba, vyote hivi ni vivutio vyenye historia ya kupendeza na kuvutia kwa wageni. Tafsiri hizi zilitolewa na wenyeji zinasema wakati wa zamani kutokana na radi kali za mara kwa mara kupiga kwenye Rasi iliyopo karibu na Ghuba hiyo na ndipo eneo likaitwa Mbamba bay.

Rasi hiyo ni kubwa na imefunikwa na uoto wa asili wa miti na nyasi, baadhi ya miti hiyo inatumika kama dawa za asili hadi nyakati hizi, watu pia hutumia msitu huo kwa matambiko ya kupiga ngoma za kufukuza au kuita majini kwa imani zao. Wanyama kama chui wakitokea milima ya Nangombo, Ukuli na Chinyemba wanapatikana katika rasi hiyo sababu kubwa ni kufuata ngedere waliopo porini humo.

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Maeneo mengine ya vivutio vya utalii kwa Wilaya ya Nyasa yaliyobainishwa ni pamoja na visiwa vya **Mbamba, Lundo, Pomonda na Hongi** ambavyo vyote vimekuwa na sifa na historia nyingi ambazo zikitangazwa vizuri zitachangia kukuza utalii kwa kuvutia watalii wa ndani na nje.

Visiwa hivi kila kimoja kimekuwa na sifa ya pekee; kisiwa cha mbamba kina sifa ya kuwa na mapango ambayo wavuvi hujihifadhi wakati wa dhoruba kali, samaki wa mapambo pia wanapatikana katika kisiwa hicho. Kisiwa cha Lundo kina historia ya kuishi wagonjwa wa ukoma waliotengwa na jamii na makaburi ya wagonjwa hao ambao walizikwa kwenye tope au kwa kugandikwa tope kwa imani kwamba wakifanya hivyo wangetokomeza ugonjwa huo. Kituo hicho baadaye kilihamishiwa kijiji cha Ngehe ambacho kipo hadi sasa.

Kisiwa kingeni ni Pomonda ambacho kina pango kubwa ambalo linaweza kuhifadhi watu zaidi ya 100 ambalo wakati huo lilitumika kujificha wakati wa vita na wavuvi kujihifadhi dhoruba inapozidi, kisiwa hiki pia ni eneo zuri ambapo hutumiwa na waogeleaji kwa ajili ya kujirusha wakati wa mchezo wa kuogelea.

Kingine ni kisiwa cha Hongi ambacho ni kidogo lakini chenye kilele ambacho kabla ya uhuru wa Tanganyika, Nchi ya Malawi wakati huo ikiongozwa na **Dkt. Ngwazi Kamuzu Banda** "Wamuyaya" iliweka Rada ambayo ilijulikana kwa jina la "Taa ya Banda".

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Mbali ya vivutio hivyo vilivyopo ziwani pia eneo la nchi kavu linabeba sehemu kubwa na muhimu katika Utalii na Uwekezaji wa Kilimo,bishara na viwanda,mabonde ya Ruhekei,Lundo na Ruhuhu yanafaa kwa kilimo cha Mpunga,tangawizi,mahindi, mbogamboga,matunda hasa mananasi, matikiti, na maembe.

Eneo la nyanda za juu za Wilaya (milimani) ambalo linajulikana kama **Umatengo** lina ardhi nzuri ambayo imekuwa ikifaa kwa kilimo cha mazao ya chakula kama mahindi, maharage na zao la biashara la kahawa ambayo ina ubora wa hali ya juu kutokana na kuzalishwa kwenye udongo wa volcano kutoka na bonde la ufa eneo ambalo linafaa sana kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo.

### **UWEKEZAJI WA VIWANDA**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Ili kuhakikisha Wilaya ya Nyasa inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kama ilivyoelekezwa na serikali ya awamu ya tano, kwa kauli mbiu inayosema "Mkoa wetu Viwanda vyetu" Wilaya imetenga eneo katika Kata ya Kilosa ambalo lina ukubwa wa ha. 56.4 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo. Miundombinu muhimu kama maji, nishati ya umeme na barabara kwa ajili ya uwekezaji huo imeendelea kuimariswa pamoja na kuanza zoezi la upimaji wa eneo.

### **MAMBOKALE**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Baadhi ya mambo hayo ni, Katika kijiji cha Mbamba bay **Rais Mstaafu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere** na **Oscar Kambona** katika harakati za kudai Uhuru walilala hapo miaka ya 1956 nyumbani kwa dada wa Oscar Kambona ambapo palikuwa na ofisi ya chama cha TANU.

Magavana wa shirikisho wa Rodesia na Nyasaland walikutana katika (Rest House) kijiji cha Mbamba bay jengo ambalo kwa sasa ni ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata wakiwa na lengo la kuagana kutokana na

vuguvugu la waafrika kudai Uhuru 1959 kushika kasi. Jengo hilo lilijengwa kwa miti.

Kuingia kwa dini na madhehebu mbalimbali pia ni sehemu kubwa ya utalii wa nyasa unaobeba historia.

Mwaka 1981 wananchi wa Lituhi waliamishwa kwa ajili ya kupisha mafuriko yaliyosababishwa na kufungwa kwa mto Shire nchini Malawi na baadaye mwaka 1987 Mwalimu Nyerere akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi alifika kwa ajili ya kutoa maamuzi magumu ya kuwarudisha katika makazi yao ya awali na baada ya kuongea na wananchi hao kwenye mti mtebhelle (muyombo) ambao upo katika kijiji cha Mwera mpya kata ya Lituhi na baadae alipiga picha na mkewe katika eneo hilo kabla ya kuondoka.

## **HISTORIA YA DINI**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Dini iliyoanza kuingia katika wilaya ya Nyasa ni dini ya Kikristo, Mwinjilisti wa kwanza wa Anglikana William Parcival Johnson alianza kuhubiri tarehe 9.2.1881 na akahamia rasmi Liuli mwaka 1906, alifariki tarehe 11.10.1928 na kuzikwa Liuli. Wakati huo ilitambulika kwa jina la Dayosis ya Nyasaland, ikafuata Southwest Tanganyika tarehe 7.7.1952 na baadaye Dayosisi ya Ruvuma tarehe 2.7.1971.

Mwinjilisti William Parcival Johnson awali wakati anaingia Nyasa alikuwa na lengo la kujenga kanisa Kijiji cha Hongi ambapo wenyeji hawakutaka na alifukuzwa ndipo akakilaani kijiji cha Hongi kiwe na sisimizi wengi, pia kiote majani yaitwayo mapelele ambayo kabla yake hayakuwapo. Historia na simulizi za wahenga zinasema hivyo.

Kanisa Katoliki liliingia mwaka 1912 huko Nkaya na kuanzisha Parokia na baadae kujenga kanisa kubwa la Lituhi mwaka 1939. Mwanzilishi akiwa ni Padre Henrich Kunster.

Uislamu uliingia Nyasa mnamo mwaka 1928, Sheikh wa kwanza aliitwa Mzee Bin Amanzi, Ilipofika mwaka 1932 Waasisi walijenga msikiti ambao mionganis mwao ni Twaib Abidallah, Akida Wabu, Mdoka, Ajali Hassan, Mfaume Bolin na Issa Kimambe.

Pamoja na wahubiri dini, Uislam uliletwa na wafanyabiashara, wavuvi na wakulima walikuja kufuata bonde la Ruhekei, Lundo na Kimbande kwa ajili ya shughuli za kilimo.

## **UTAMADUNI.**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Utamaduni ni eneo lingine ambalo linachangia sana kukuza utalii wa mahali popote. Watu walioishi miaka mingi iliyopita Wilaya ya Nyasa walicheza ngoma mbalimbali zikiwa na lengo la kuburudisha, kuelimisha, kukosoa au kuwapongeza watu mbalimbali waliofanya mambo mazuri kwa jamii. Ngoma hizo ziliitwa Mganda (ngoma hii ilichezwa na wanaume), Kioda (walicheza akina mama). Ngoma nyingine kama vile Lindeku, Mhambo, Lingoga na Chomanga walicheza mchanganyiko wanaume na wanawake.

Vyakula ni sehemu kubwa ya utalii vyakula vya asili kwa wakazi wa Nyasa vimegawanyika katika makundi yafuatayo; chakula kikuu ni ugali wa mihogo, mahindi, ulezi, mtama na ngano, vitoweo ni vimegawanyika katika makundi manne yafuatayo; samaki wakubwa na wadogo pamojana na dagaa.

Kundi la pili mboga za majani ikiwemo mlenda, kisamvu, mchicha asili (libonongo) nk kundi jingine ni wadudu kumbikumbi, likungu, chenene (makururu), manyege au viyenje, mbambwa (majimoto) manganiwa na nk.

## **HIFADHI YA MAZINGIRA**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Wilaya inafanya jitihada kubwa ya uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na ufugaji nyuki, utunzaji wa misitu, upandaji miti ya asili, hifadhi ya vyanzo vya maji, upandaji miti kibiashara, matunda kama machungwa, malimao, korosho na maembe.

Wilaya ina pori ya akiba la wanyama pori la Liparamba ambalo lila wanyama wengi wakiwemo tembo, simba, chui, nyati, ngolombwe, parahala, tandala wakubwa, pundamilia, nyani manjano, pongo, Ngiri, pofu, kuro, fisi, nguruwepori, nk, pamoja na ndege jamii mbalimbali

zaidi ya aina 80 ambaao ni kivutio kizuri kwa watalii, Wanyama wa pori hili katika majira **fulani** ya mwaka wanatabia ya kuhama kwenda nchi jirani ya Msumbiji baada na baadaye hurudi tena kwenye pori letu la Liparamba.

Kadhalika pori hili lina maporomoko ya maji ya mto Ruvuma ambaao umepita humo na unapokea maji kutoka mito miwili ya Lunyele na Lumeme ni kivutio kikubwa cha utalii na uwekezaji katika sekta hiyo.

## **HUDUMA ZA JAMII**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Huduma nyingine za jamii ambazo zimeendelea kuimariswa ni kuwaongoza na kuwatunza watalii, makampuni ya usafirishaji, Maeneo yanayoweza kupokea wageni na kupata huduma muhimu za Kupumzika, chakula, malazi na kubarizi ni Bio Camp, Pomonda Camp, Mharo Beach Hotel, St. Vincent Seminas House, Linda Camp, St Bernadetha Sisters Hotel.

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Katika kuadhimisha siku ya utalii mwaka huu Wilaya kwa kushirikiana na taasisi za kitaifa imeendesha mafunzo ili kuwajengea uwezo wajasiriamali. Mafunzo hayo ni kama yafuatayo;

- Chuo cha Taifa cha Utalii chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kiliendesha mafunzo ya Ukarimu na Utalii kwa watu 137 watoa huduma wa migahawa, hoteli na nyumba za kulala wageni mafunzo hayo yalianza tarehe 27 hadi 31 Desemba 2017.
- BRELA walifanya mafunzo ya namna ya uanzishwaji na usajili wa biashara kutoka wakala wa usajili wa biashara na leseni BRELA kuanzia tarehe 4 hadi 5 Januari 2018 ,
- Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) waliendesha mafunzo ya teknolojia ya usindikaji wa Muhogo na bidhaa zake, kusindika matunda, usalama na ubora wa vyakula, ufungashaji wa dagaa na uwekaji nembo ya bidhaa kutoka SIDO kuanzai tarehe 2 hadi 6 Januari 2018,
- Mafunzo ya Usalama barabarani kutoka kikosi cha usalama barabarani Mkoa wa Ruvuma na Mamlaka ya Mapato ili kuwawezesha waendesha bodaboda na vyombo vingine vya usafiri kuzifahamu sheria na taratibu za usalama barabarani na majini.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wakazi wa Nyasa wanaojishughulisha na kutoa huduma mbalimbali kwa jamii waweze kuwapokea na kuwaongoza watalii wetu wanapoingia na kutoka ndani ya wilaya yetu.

## **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA UTALII KATIKA WILAYA YA NYASA.**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Changamoto zinazoikabili sekta ya utalii katika wilaya ya Nyasa ni;

- Ukosefu wa wataalamu wa mambo ya utalii, hivyo kunapelekea kudhorotesha sekta ya utalii katika wilaya yetu.
- Ukosefu wa miundombinu bora kama barabara za ndani, viwanja vya ndege katika wilaya, vitakavyoweza kuunganisha wilaya ya Nyasa na wilaya zingine na Nchi kwa ujumla.
- Ukosefu wa wawekezaji binafsi wa makampuni ya utalii katika Wilaya yatakayotoa huduma za kitalii kwa watu mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.
- Vivutio vya utalii havijatangazwa ndani na nje ya nchi kwa sababu hakuna Taasisi inayojishughulisha na kuelekeza au kutangaza vivutio vilivyopo.
- Uelewa mdogo wa jamii katika maswala ya utalii na utunzaji wa mazingira.

## **MIKAKATI**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

- Wilaya imeendelea kutenga nafasi ya mtaalam wa utalii na kuomba toka serikalini.
- Wilaya katika jitihada za kutunza mazingira ya utalii yawe mazuri wananchi wote wamekuwa wakishirikishwa kufanya usafi katika ziwa na fukwe ziwe safi ili kuwavutia watalii na wawekezaji
- Wilaya inaendelea kuhifadhi safu za Milima ya livingstone iwe kijani pale pasipokuwa na miti papandwe miti ili kurejesha hali ya kijani na hewa safi kwa kushirikisha wadau wengine
- Wilaya inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wavuvi wetu kwa kuhamasisha wavuvi kutengeneza boti za kisasa na kuwaelimisha wavuvi juu ya uvaaji vifaa vya usalama ili kulinda usalama wao wawapo majini.

- Wilaya inaendelea kulinda maeneo ya kihistoria na kiutamaduni kwa kushirikisha wananchi.
- Wilaya inaendelea kuifanya Wilaya ya Nyasa kuwa kitovu cha utalii. Aidha alipotembelea aliyekuwa Waziri wa maliasili na utalii Profesa Jumanne Magembe alisema wizara yake ina mpango wa kuifanya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma kuititia vivutio vyake vya utalii kuwa kitovu cha utalii kusini mwa Tanzania ili kuchangia pato la taifa kuititia utalii
- Wilaya inaendelea kushirikisha sekta binafsi kwenye utalii
- Wilaya inaendelea na hatua mbalimbali kuvitangaza vivutio mbalimbali vya utalii hasa kwa wananchi ili kutoa fursa kwao kuvilinda na kuviifadhi kwa manufaa yao.
- Wilaya inafanya jitihada za kutumia vyombo vya habari kushirikishwa katika kuelimisha, kufundisha na kuburudisha umma wa watanzania ili wafahamu utalii wa kiutamaduni na kii kolojia kwa ujumla.

## **HITIMISHO**

### **Mhe. Waziri Mkuu,**

Wilaya ya Nyasa bado ina fursa za maliasili ya kutosha (misitu, wanyamapori, samaki, mito, ziwa, fukwe na mali kale) ambazo hazijaharibiwa na hivyo zinaweza kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa na wananchi kuititia utalii wa kiutamaduni na ikolojia. Kwa kuendelea kulitangaza Tamasha letu la utalii kwa kila mwaka katika Wilaya Nyasa.

Naomba kuwasilisha

**ISABELA O. CHILUMBA  
MKUU WA WILAYA YA NYASA**